easytvet.com

Jina la Mtahiniwa: ______________________ Nambari: ____________/________

7015/2
LUGHA YA KISWAHILI
Disemba 2016
Saa: $1\frac{1}{2}$ hours

Sahihi ya Mtahiniwa: ______________

Tarehe: ______________

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT AND EDUCATION

LUGHA YA KISWAHILI

**Saa $1\frac{1}{2}$**

**MAAGIZO**

*Andika namba na jina lako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Tia sahihi yako na tarehe kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Mtihani huu una sehemu tatu:* ***Insha****,* ***Ufahamu*** *na* ***Matumizi ya Lugha****.*
*Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*
***Andika majibu yote kwa lugha ya Kiswahili.***

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| I | 15 | |
| II | 15 | |
| III | 20 | |
| JUMLA | 50 | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2016 The Kenya National Examinations Council.

easytvet.com

## SEHEMU YA KWANZA: INSHA (alama 15)

*Jibu swali la **1** au la **2**.*

*Andika insha isiyopungua maneno 300 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:*

1. Kiongozi nimpendaye.

2. Maliza insha yako kwa maneno yafuatayo:

   ... "ndipo nilipotambua kuwa subira huvuta heri."

easytvet.com

## SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (alama 15)

3. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Mwanamke ni nguzo katika jamii tangu jadi. Majukumu yake **hayakadiriki**; hunadhifisha nyumba, hupika, hulea watoto na kuiunganisha jamii kupitia kwa miradi mbalimbali miongoni mwa majukumu mengine. Aidha wao huwajibika kutunza mimba kwa miezi tisa na kuhimili uchungu wa kujifungua. Japo mwanamke ana dhima hii muhimu katika jamii, amekabiliwa na changamoto si haba.

Ukeketaji wa wasichana huwaathiri kwa njia nyingi. Vifaa na mbinu za ukeketaji huogofya. Isitoshe, usafi wa vifaa hivi hutiliwa shaka kwa sababu vinaweza kusababisha maradhi ya kuambukiza ukiwemo ugonjwa sugu wa UKIMWI. Hali kadhalika, hakuna mbinu yoyote ambayo hutumiwa kuwapunguzia uchungu wala kuzuia kuvuja damu. Huenda wakakabiliwa na hatari ya kifo.

Wakati majanga kama vile vita vya kikabila, ghasia za kisiasa, migomo na wizi wa kimabavu yanapotokea katika jamii, wanawake ndio wanaoathirika pakubwa kwa kubakwa. Kitendo hiki cha kinyama kina madhara makubwa kwa mwanamke. Kuna uwezekano wa kupata mimba zisizotakikana, kuambukizwa maradhi ya zinaa, kuumizwa kimaumbile na kusababishiwa unyanyapaa.

Suala nyeti la ndoa za mapema kwa wasichana wa umri mdogo, ni tishio kubwa kwa ustawi wa jamii. Hali hii huwadunisha wasichana kiasi cha kuonekana kama bidhaa za kunadiwa sokoni. Wazazi wa wasichana hawa hupokea mahari mapema hata bila idhini ya wahusika; jambo ambalo linawalazimisha kuwaoza mara tu wanapokeketwa. Ndoa hizi zinaathiri masomo na maendeleo ya wasichana hawa kwa njia **hasi**.

Jamii nyingi huwabeza wajane kana kwamba hawana haki zao. Baadhi yao hulazimishwa kurithiwa kinyume na mapenzi yao. Hali hii inazua migogoro katika familia na huenda mwanamke akaambukizwa magonjwa hatari kiasi cha kutoweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Jamii inawawekea vikwazo wajane kama vile haiwatarajii waolewe tena. Wajane ambao wamerithiwa wakiwa tayari wamefunga uzazi wanakabiliwa na masimango makali kutoka kwa jamii inayotarajia watoto. Wengine wao hunyang'anywa mali ya waume zao na jamaa za waume hao.

Wanawake hawajapewa kipaumbele katika masuala ya urithi wa mali. Wazazi wengi huwarithisha mali watoto wa kiume na kuwanyima wasichana. Mazoea haya huwaacha wasichana **wakilia ngoa** kwa sababu wanahisi wamebaguliwa. Hata hivyo, katiba mpya ya mwaka 2010 inawatetea kwa kuwapa haki ya kurithi mali kwa kiwango sawa na wanaume.

Licha ya wanawake kukabiliwa na pingamizi hizi zote, wana nafasi ya kujikomboa na kusimama kidete kutetea haki zao wenyewe.

easytvet.com

**Maswali**

(a) Thibitisha kwa kauli **tatu** kuwa mwanamke ni nguzo katika jamii. (alama 3)

(b) Eleza athari **tatu** zinazotokana na tohara ya wasichana. (alama 3)

(c) Kulingana na kifungu, taja mazingira **mawili** yanayoweza kusababisha kudhulumiwa kwa mwanamke kimapenzi. (alama 2)

(d) Kwa kurejelea aya ya **tano**, eleza haki **tatu** za wajane. (alama 3)

(e) Katiba mpya ya mwaka wa 2010 imewanufaisha vipi wanawake? (alama 1)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu.

(i) Hayakadiriki ____________________ (alama 1)

(ii) Hasi ____________________ (alama 1)

(iii) Wakilia ngoa ____________________ (alama 1)

easytvet.com

## SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (alama 20)

*Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.*

4. (a) Tunga sentensi moja ili kutofautisha maneno yafuatayo: (alama 2)

   (i) Sharti;
   (ii) Shati.

   ______________________________

   ______________________________

   (b) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wastani. (alama 2)

   Majilima yale yanafuka moshi.

   ______________________________

   ______________________________

   (c) Sahihisha sentensi hii kwa njia **tatu** tofauti. (alama 3)

   Humu ndiko anapoishi.

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   (d) Tunga sentensi sahihi kudhihirisha matumizi ya kivumishi kimilikishi. (alama 2)

   ______________________________

   ______________________________

   (e) Unda kitenzi kutokana na kielezi kifuatacho. (alama 1)

   Haraka ______________________________.

   (f) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

   "Pitia kwetu hapa uchukue mayai." Rafikiye alimwambia.

   ______________________________

   ______________________________

easytvet.com

(g) Tambua kiunganishi katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Anapenda kusoma sana kwa kutaka kufaulu.

(h) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 3)

Nomino + Kivumishi + Kitenzi

______________________________________________

(i) Akisami moja kwa nane huitwa ________________________. (alama 1)

(j) Riadha ni jumla ya michezo ya ________________________, kukimbia na ________________________. (alama 2)

(k) Panda ni ________________________ pia ni kuweka mbegu ardhini. (alama 1)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**